WARUMI

MAJIBU YA MITIHANI



shepherds
GLOBAL CLASSROOM

WARUMI

MAJIBU YA MITIHANI

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Somo la 1
Utangulizi wa Barua

(1) Je, kwa nini Paulo aliandika waraka kwa Warumi kwa waamini wa Rumi?

Ili kujitambulisha na kuitambulisha teolojia yake kuhusu wokovu kwa waamini wa kirumi akiwa na lengo la kuwatembelea na kuanza kazi mpya ya umisheni kwa msaada wao.

(2) Je, kwa nini Paulo alipanga kwenda Rumi?

Paulo alitaka kulitumia kanisa katika Rumi kama kituo chake cha kuzindulia jitihada zake za umisheni za kuingia Hispania

(3) Je, Maana ya msemo *Yesu Krsito Bwana wetu* una maana gani katika nyaraka za Agano Jipya?

Linasema kwamba yeye ni mtu wa kihistoria aliyeitwa Yesu, yeye ni Masihi wa Kiyahudi, na yeye ni Mungu.

(4) Je, ufufuo unathibitishaje uungu wa Yesu?

Mtu ambaye siyo Mungu hawezi akajifufua mwenyewe kutoka katika wafu; aidha Mungu hangeweza kumfufua mtu anayejinadi kwa upotofu kwamba yeye ni Mungu.

(5) Elezea msemo *wasio wayunani* (Warumi 1:14).

Ni watu ambao hawakuwa wayunani walikuwa ni wageni, wasio tokana na utamaduni wa Wayunani.

(6) Kwa nini Mwinjilisti Paulo ana deni la kuhubiri injili?

Mwinjilisti ana deni la injili kwa waliopotea kwa sababu Mungu alisema tuitoe kwao.

(7) Je, ni kitu gani kikuu na ukweli muhimu katika kitabu cha Warumi?

Mtu anafanywa mwenye haki kwa Imani na ataishi kwa imani.

(8) Je, kifo kina maana gani katika kitabu cha Warumi?

Maana yake ni hukumu ya Mungu

(9) Kulingana na Warumi, ni nani analindwa asipate hukumu ya Mungu?

Ni wale tu ambao wamehesabiwa haki kwa imani

Somo la 2
Kosa la Wamataifa

(1) Je, ni kwa njia gani watu hupokea ufunuo wa Msingi?

Kwa kutazama uumbaji wa Mungu

(2) Je, watu wote wanajuaje kuhusu Mungu hata bila Maandiko?

Watu wanajua kwamba Mungu yupo, na kwamba wanapaswa kumtii, na kwamba wamekwisha mwasi..

(3) Je, Ufunuo maalumu ni nini?

Ni ukweli uliofunuliwa katika Biblia na katika Kristo kuvaa mwili

(4) Je, kuabudu sanamu ni nini?

Ni kutumikia na kuabudu kitu ambacho Mungu alikiumba.

(5) Taja njia mbili ambazo zinaleta madhara ya upotovu wa fikira kwa watu

- Huzuia watu wanapohitajika kufanya uamuzi katika masuala ya maadili
- Husababisha watu kutetea tamaa za dhambi na vitendo vyake.

Somo la 3
Kosa la Waisraeli

(1) Je, Maandiko yanayohusu siku za mwisho yanaelezaje?

Yanaelezea muda ambao Mungu kwa ghafla ataingilia kati duniani, akiadhibu uovu na akiwasaidia watu wake.

(2) Je, kwa nini Wayahudi walitarajia kupata Upendeleo?

Walidhania kwamba walikuwa wamependelewa na Mungu kwa sababu walikuwa ni uzao au watoto wa Ibrahimu.

(3) Je, mtu anahesabiwaje haki?

Mtu anakuwa mwenye haki kwa neema kwa njia ya imani.

(4) Je, mtu huoneshaje kwamba anayo imani iokoayo?

Mtu huonesha kuwa anayo imaini iokoayo kwa kuishi kwa uaminifu.

(5) Je, tohara ina umuhimu gani kwa Myahudi, na ina mfano gani kwa Mkristo?

Tohara ilikuwa ni alama ya kumtambulisha Myahudi, kuthibitisha kuwa alikuuwa ni miongoni mwa watu wa Mungu. Kwa Mkristo ni ishara ya kazi ya Roho Mtakatifu kubadilisha moyo wa mwenye dhambi ili aweze kumpenda na kumtii Mungu.

Somo la 4
Hali ya Ulimwengu Wote

(1) Elezea dhana ya Calvin ya "neema ya kawaida".

Aliamini kuwa Mungu huwapa watu wote neema ambayo huwawezesha kufanya mambo mazuri. Hakuamini kuwa neema ya kawaida inamletea mtu wokovu.

(2) Elezea dhana ya Wesley ya "neema ya awali" yaani neema inayotangulia.

Mungu huwapa watu hamu na uwezo kuitikia lakini kuna uwezekano watu kupinga. Mungu huweka uwezekano wa mtu kuchagua. Hii ni neema ya kwanza inayokuja kwa kila mtu.

(3) Katika Warumi 3:19, maneno "kila kinywa kufumbwe" yana maanisha nini?

Yana maana kuwa hakuna mtu mwenye udhuru au msingi wa kujihesabia haki.

(4) Je, ni manufaa gani mabwa yanatajwa kwa Wayahudi katika Warumi 3?

Walikuwa wa kwanza kupokea Maandiko.

(5) Je, aina mbali mbali za kuabudu zinatunufaishaje?

Ni aina zilizopo kutusaidia imani yetu. Tunapozifanya kwa imani, tunapata neema.

(6) Je, Warumi 3:10-18 inaonesha nini?

Hakuna mwenye haki bila kuwa amepokea haki ya Mungu.

(7) Je, ni nani aliyeko chini ya sheria? (Warumi 3:19-20)

Ni mtu ambaye hufikiri kuwa ni lazima kushika sheria ili kukubaliwa na Mungu.

Somo la 5
Njia na Maana ya Kuhesabiwa Haki

(1) Je, Mtu aliye na imani iokoayo anaamini nini?

- Anaamini kwamba hawezi kufanya lolote katika kujihesabia haki mwenyewe.
- Anaamini kwamba dhabihu ya Kristo inatosha kwa ajili ya msamaha wake.
- Anaamini kwamba Mungu atamsamehe yeye kwa sharti la imani peke yake.

(2) Je, ni tatizo gani lilitatuliwa na upatanisho?

Mungu kumhesabia haki mwenye dhambi na bado aendelee kuwa mwamuzi mwenye haki.

(3) Ni jinsi gani upatanisho ulitatua tatizo?

Mungu alitoa dhabihu kama msingi wa msamaha. Anaweza kumsamehe mtu aaminiye, lakini dhabihu huonesha kuwa Mungu huzichukulia dhambi kwa uzito wa hali ya juu sana.

(4) Je, kuhesabiwa haki ina maana gani?

Kuhesabiwa haki inamaanisha kwamba mwenye dhambi anayetubu na kuamini anahesabiwa kuwa mwenye haki kama ambaye hajawahi kufanya dhambi tena.

(5) Je, ni kwa njia gani mtu anaiheshimu sheria kama kipimo cha kuhesabiwa haki?

(Warumi 3:31)

Kwa kutubu dhambi na kuishi kwa utii.

(6) Je, ahadi ya Mungu ya neema kwa Abraham ilikuwa ni nini?

Kwamba kupitia uzao wako neema ya Mungu itatolewa kwa watu wote wa dunia.

(7) Je, Daudi alisemaje kuhusu kuhesabiwa kwa imani?

Aliielezea kuwa ni kukubaliwa na Mungu kunakofanywa msamaha wa dhambi

(8) Je, nani ni watoto wa kiroho wa Ibraham?

Ni watu walio na imani iokoayo

(9) Tunajua nini kutoka katika Warumi 5:15 kwamba wokovu hutolewa kwa kila mmoja?

Aya hii inasema kwamba kama vile dhambi ya Adamu ilivyosababisha kila mtu akawa mwenye dhambi, upatanisho wa Kristo unatoa neema kwa kila mtu.

Somo la 6
Ushindi dhidi ya Dhambi

(1) Je, kwa nini ni muhimu kuelewa dhambi ni nini?

Ili tuweze kuelewa toba na ushindi, ni lazima tuelewe dhambi ni nini.

(2) Je, maana ya dhambi ya kukusudia ni nini?

Wakati mtu anapofanya kwa kukusudia na kwa kujua akachagua kutokumtii Mungu, hiyo ni dhambi ya kujitakia au hiari.

(3) Ni dhana gani potofu ambayo Paulo anaijibu katika Warumi 6?

Kwasababu ya neema, waamini hawahitaji kuishi katika utii wa sheria za Mungu.

(4) Je, kuifia dhambi ina maana gani?

Kuwa mfu katika dhambi ni kutokuwa tena chini ya nguvu za dhambi au kuthibitiwa nayo.

(5) Je, ina maana gani kuwa chini ya neema?

Kuwa chini ya neema ina maana kuwa unategemea neema ili kukubaliwa na Mungu.

(6) Je, kuwa chini ya sheria ina maana gani?

Kuwa chini ya sheria ina maana kuwa unategemea kuitii sheria ili ukubaliwe na Mungu.

(7) Je, kwa nini ni haiwezekani kumtumikia Mungu na dhambi?

Haiwezekani kutumikia kwa pamoja Mungu na dhambi kwa sababu wewe ni mtumishi kwa yule unayemtii. Kama utaitii dhambi, dhambi ndiyo bwana wako; ikiwa na maana kwamba Mungu siyo Bwana wako.

(8) Je, msemo wa utu wa kale maana yake ni nini?

Utu wa kale ni maisha ya kibinafsi ya dhambi ambayo mwenye dhambi anaachana nayo wakati anapokuwa ameamini na kuokoka.

Somo la 7
Mtenda Dhambi Mwenye Hatia

(1) Taja sababu mbili zinazonesha kuwa sheria za ibada na sheria za kiraia za Agano la kale bado zina umuhimu.

- Zinadhihirisha asili ya Mungu, ambazo kamwe hazibadiliki.
- Zinatoa kanuni za maadili za kutumiwa katika njia maalumu.

(2) Je, ina maana gani kufa katika sheria?

Kuwa umekufa kwa sheria hatuhitajiki kuitimiza kama njia ya kuhesabiwa haki, kwa sababu tumehesabiwa haki kwa njia ya neema.

(3) Je, neno *katika mwili* lina matumizi gani mawili?

- Ni kuwa tu katika hali ya kibinadamu, ya kufa.
- Ni kutawaliwa katika anguko la hali ya asili ya dhambi.

(4) Je, sheria inafanyaje dhambi iwe mbaya Zaidi?

Mwenye dhambi anapoona kuwa ni mkosaji, dhambi zake anazoendelea nazo (kutokutii sheria ya Mungu) hapo huwa anajua hali yake ya uasi.

(5) Kwa nini sheria inafaa kwa uinjilisti?

Mtu anaona hitaji lake la wokovu anapotambua kwamba ana hukumiwa na sheria ya Mungu.

Somo la 8
Maisha katika Roho

(1) Kwa nini haiwezekani sheria iwe ni njia ya wokovu?

Mwenye dhambi hakufuata sheria.

(2) Je, ina maana gani kusema mwamini hatawaliwi tena na mwili?

Mwamini hatawaliwi na mwili na ana nguvu za kushinda majaribu.

(3) Je, ni kwa jinsi gani sheria inaelekeza maisha ya mkristo?

Inaonesha jinsi Mungu anavyotaka tuishi.

(4) Je, ushuhuda wa Roho ni nini?

Roho wa Mungu anatuthibitishia kwamba tuko kwenye uhusiano wa upendo na utii pamoja na Mungu na ni shuhuda kwamba tumeokoka.

(5) Wokovu wa mwisho ni nini?

Mwisho wa yote, urejeshaji mkamilifu wa uumbaji utakuwa

(6) Je, kama watu watakana ufufuo wa mwili matokeo yake ni nini?

Maisha ya kujinyima (msimamo mkali wa kukandamiza tamaa za kimwili kwa sababu walifikiri kuwa wao ni waovu) au ufuatiliaji wa raha (msimamo wa uzembe na kudekeza tamaa za mwili kana kwamba hazina madhara yeyote)

(7) Je, ni nini usalama wa mwamini?

Usalama wa mtu aliyeokoka ni ahadi ambayo kamwe Mungu hawezi kushindwa kumpa nguvu ya kuvumilia katika imani yake na hakuna nguvu nyingine yeyote itakayoweza kumtoa kutoka kwa Mungu.

Somo la 9
Uteuzi wa Mungu

(1) Je, tunajuaje kuwa Mungu anataka tuelewe anavyotenda haki?

Mungu ameelezea sera zake za wokovu, akielezea ni kwa nini ni za haki.

(2) Je, ni kwa nini ni muhimu kwetu kuona kwamba Mungu ni wa haki?

Itakuwa ni jambo lisilowezekana kwetu sisi kumwabudu Mungu katika kweli kama hatutamwona yeye kuwa ni mwenye haki.

(3) Je, mtazamo wa kibiblia kuhusu ukuu wa Mungu ni upi?

- Mungu amechagua kuruhusu watu kufanya chaguzi za kweli pamoja na matokeo yake.
- Mungu huwaacha watu wakae na chaguzi zao walizozifanya
- Mungu ni mwenye nguvu na hekima ya kutosha katika kukamilisha mpango wake wa mwisho licha ya yale ambayo mtu mwingine yeyote anayafanya.

(4) Je, jambo kuu katika Warumi 9 ni nini?

Mungu amechagua njia ya wokovu, na hakuna njia nyingine yeyote ambayo mtu anaweza akaitumia katika kupata wokovu.

(5) Je, manufaa ya kiroho ya Israel ni nini?

- Kwanza walikuwa na Mungu kama Baba.
- Kwanza walikuwa wameuona utukufu wa Mungu ukifunuliwa.
- Walikuwa na:
  - Maagano kama masharti ya baraka zake.
  - Sheria.
  - Aina za kuabudu.
  - Ahadi za wokovu mkuu.
- Mababa wa ahadi walikuwa Wayahudi.
- Yesu alizaliwa kama Myahudi.

(6) Je, kuna mahusiano gani matano kati ya Ukristo na Uyuda?

- Wakristo na wafuasi wa Uyahudi wote kwa pamoja wanamwabudu Mungu mmoja wa kufanana na wamepokea ufunuo kutoka kwa Mungu
- Uyahudi ndio uliotoa msingi wa teolojia na falsafa ya Ukristo
- Wakristo na wafuasi wa Uyahudi wanakubaliana na Agano la Kale kama ndiyo Maandiko, lakini wafuasi wa Uyahudi hawakubaliani na Agano Jipya.
- Yesu, mwanzilishi wa Ukristo, alikuwa ni Myahudi na aliithibitisha dini ya watu wake.
- Moyo wa Uyahudi ulikuwa unamtarajia Masihi. Wakristo wa kwanza walikuwa ni Wayahudi ambao waliamini kwamba Yesu alikuwa ndiye Masihi.

(7) Je, Warumi 9 inasemaje kuhusu Mungu kumchagua Yakobo?

Wakati Mungu alipomchagua Yakobo badala ya Esau, hakuwa akichagua mtu yupi wa kuokoa. Alihitaji kuchagua yule ambaye ataweza kumtumia katika kutimiza mpango wa wokovu

(8) Je, kwa nini tunafurahia ukuu wa Mungu?

Tunaweza tukafurahia katika ukuu wa Mungu kwa sababu kila siku ni mwenye hekima, ni mzuri, ni mwenye upendo na haki katika kila analolitenda.

Somo la 10
Ujumbe wa Haraka

(1) Je, jambo kuu katika Warumi 10 ni nini?

Haki ni lazima ipatikane kwa imani, na umuhimuwa imani uhafanya ujube wa injili uwe na umuhimu wa haraka.

(2) Je, ni jinsi gani Wayahudi walijaribu kujihesabia haki?

Kwa kuanzisha kumbu kumbu mahususi za haki binafsi.

(3) Je, tunajuaje kuwa watu walioishi kabla ya Kristo kuja walikuwa hawaokolewi kwa njia ya matendo?

Paulo anaelezea waziwazi kwamba watu wote waliojaribu kutengeneza haki yao wenyewe kwa njia ya matendo walikuwa wamepotoshwa na kupotea.

(4) Je, ina maana gani kuwa wokovu uko mioyoni na midomoni mwetu?

Tumeupokea kwa imani (mioyoni mwetu) na kukiri (kwa vinywa vyetu).

(5) Je, ni kwa nini ujumbe wa mishenari ni wa haraka?

Kwa kuwa watu wanaokoka kwa imani, wanahitaji kusikia ujumbe ambao utawapeleka katika kuamini.

(6) Elezea mfano wa matawi ya mti katika Warumi 11.

Waisraeli walikuwa kama ni matawi yaliyokatwa kutoka kwenye mti wa Mungu, na Wamataifa kama matawi yaliyoongezwa kwenye mti huo, ambayo hayakuwa sehemu ya mti hapo awali. Wayahudi walikatwa kwa sababu ya kutoamini kwao. Mtu yeyote aliyeletwa katika mti huo atakatiliwa mbali pia kama hataendelea kuwa ndani ya imani katika mti huyo. Wale ambao walikataliwa mbali wanaweza pia wakarejeshwa tena.

(7) Orodhesha aina tatu za ahadi za Agano la Kale.

- Ahadi za Wokovu
- Ahadi za Mungu za utunzaji wa watu wake.
- Ahadi kwa Israeli kama Taifa.

Somo la 11
Huduma na Mahusiano

(1) Elezea mfano wa dhabihu iliyo hai.

Tumejitolea kabisa kama dhabihu inayopaswa kuuawa, lakini badala ya kufa, tunaishi kwa ajili ya Mungu. Hiyo ina maana kwamba msimamo huo ni lazima uzingatiwe. Mfano wa dhabihu iliyo hai unasisitiza kujitoa kwetu kabisa kama sadaka.

(2) Je, nini lazima itokee kwetu ili tuweze kuwa waminifu kwa Mungu?

Ni lazima tubadilishwe kwa kufanywa upya nia zetu.

(3) Je, ni kwa nini inatupasa kuwa wanyenyekevu?

Kila kitu tulicho nacho tumepewa na Mungu.

(4) Elezea msemo wa *ndugu aliye dhaifu* na *ndugu aliye na nguvu*.

Ndugu mdhaifu ni yule anayejihisi kuwa na hatia katika kitendo ambacho kiuhalisisia hakijawahi kukatazwa na Mungu. Ndugu thabiti ni yule anayafanya kitendo bila kujihisi kuwa na hatia kwa sababu anajua kwamba kitendo anachokifanya kiuhalisia hakihusiki kabisa katika kukosa utii kwa Mungu.

(5) Nani walikuwa wanaotetea ufuatwaji wa sheria za Kiyahudi?

Hawa ni Wayahudi waliojinadi kuwa wao ni Wakristo lakini wakafikiri kwamba Wakristo ni lazima pia watekeleze matakwa ya dini ya Uyahudi.

Somo la 12
Maono kwa Ajili ya Umisheni

(1) Elezea jinsi tamaduni kuu tatu zilivyotayarisha ulimwengu kwa ajili ya kuenea injili katika karne ya kwanza.

Mwanafunzi lazima aorodheshe baadhi dondoo zinazopatikana katika somo hili kuhusu utamaduni wa wayunani, warumi, na wayahudi.

(2) Je, mtu anaoneshaje kuwa Mungu wakati wote alipanga injili iende kwa Wamataifa?

Manabii walitabiri kuwa

- Watu wa Mataifa watakuwa watu wa kumwabudu Mungu
- Masihi atatawala juu ya watu wa Mataifa.
- Watu wa Mataifa watamtumainia Masihi.

(3) Je, ni kwa nini sadaka ya kanisa ilikuwa muhimu sana Yerusalemu?

Kwa kuituma hiyo sadaka, Wamataifa walikuwa wanakiri dhamana waliyo nayo kwa Wayahudi kwa sababu Wayahudi waliogeukia Ukristo ndio waliowaletea injili. Kwa kuipokea ile sadaka, Wayahudi wanakiri kwamba Wamataifa walikuwa sawa na wao katika kanisa moja.

(4) Je, Paulo alifikaje Rumi?

Paulo aliwasili Rumi kama mfungwa baada ya kukamatwa huko Yerusalemu na kuwekwa mahabusu na watawala wa Kiyahudi, akachukuliwa na gavana wa Kirumi, na mwishowe akapelekwa Rumi kwa mashtaka.

Kristo-katikati. Mafunzo. Kila Mahali.

SHEPHERDSGLOBAL.ORG